



# WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI (RITA)



## TAARIFA KWA UMMA

### MAELEKEZO YA KUVAA BARAKOA (MASK) UNAPOFIKA KUPATA HUDUMA KATIKA OFISI ZA RITA

Uongozi wa RITA unapenda kuwakumbusha wananchi kuzingatia maelekezo ya Serikali na Wataalamu wa afya kuhusu kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Corona (COVID 19) ikiwa ni pamoja na kuvaa **BARAKOA** wanapofika kupata huduma katika ofisi za Wakala nchi nzima.

Aidha, tunawashauri wananchi kuendelea kutumia njia mbadala za mawasiliano ili kupata taarifa mbalimbali na huduma zinazotolewa na Wakala. Njia hizo ni pamoja na:

- Kupiga simu( **Bila malipo**) namba [0800 117 482](tel:0800117482)
- Tovuti: [www.rita.go.tz](http://www.rita.go.tz)
- Barua pepe: [info@rita.go.tz](mailto:info@rita.go.tz)
- Facebook: [facebook@ritatanzania](https://www.facebook.com/ritatanzania)

Fomu za maombi ya huduma zetu zote zinapatikana katika tovuti ya wakala iliyotajwa hapo juu.

RITA tunaendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA ili huduma nyingi zaidi ziweze kupatikana bila kufika Ofisi za Wakala hasa katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona.

***“Pamoja tushirikiane kupambana na Corona”***

Imetolewa na :

**Kitengo cha Masoko na Mawasiliano**

Jumanne, Aprili 21, 2020